ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.

24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.

35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.

50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.

70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

(Kikao cha Tisa – Tarehe 27 Oktoba, 2009

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Ali Mzee Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 20

Kambi za Vijana

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Katika kuratibu uhusiano na ushirikiano wa vijana mbali mbali ndani na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuendeleza kambi za vijana, Idara ya Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na vijana wa UVIKIUTA wa Tanzania Bara wameweza kuteua vijana sita (6) watakaojiunga na kambi za vijana za kimataifa kwa mwaka 2009/2010. Kati ya vijana hao watatu wamefanikiwa kushiriki katika kambi hizo; mmoja Kenya, mmoja Canada na mmoja Ujerumani.

(a) Je, Mhe. Waziri vijana hawa wametoka katika wilaya gani kwa Unguja na Pemba na ni wa jinsia gani?
(b) Je, Mhe. Waziri vijana wanateuliwa vipi kutoka ngazi za chini na kwa sifa zipi?
(c) Je, sisi Zanzibar tumeshapokea wageni wa kimataifa toka nchi gani?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya mwanzo kwa leo hasa tukiwa tunatoka kiwanjani kumpokea Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Amani Abeid Karume aliyekuja na barka ya mvua.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kujibu swali la Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Wizara yangu kwa muda mrefu inashirikiana na UVIKIUTA ya Dar es Salaam kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa vijana wa Zanzibar na nchi mbali mbali duniani kupitia Kambi ya Kazi za Vijana.

Ni kweli kwa mwaka huu vijana sita (6) wa Zanzibar walipata fursa ya kushiriki Kambi Kazi za Vijana nchini Kenya, Canada, Ujerumani, Ireland na Ureno.

(a) Kati ya vijana hao sita (6), vijana wanne (4) walikwenda Kenya na kati ya hao wanne (4) waliokwenda Kenya, kijana mmoja wa kiume alitoka Wilaya ya Mkoani na kijana aliyekwenda Canada alitoka Wilaya ya Mkoani. Vijana watatu (3) waliobaki ambao walikuwa miongoni mwa wale vijana wanne (4) waliokwenda Kenya walitoka Mkoa wa Mjini Magharibi. Aidha, kijana mmoja (1) ambaye alikwenda Ujerumani, Ireland na Spain anatoka Mkoa wa Mjini Magharibi, Wilaya ya Magharibi.

(b) Vijana hawa wanateuliwa kutoka katika maeneo yanayofanyika Kambi Kazi. Uteuzi unafanywa wakati wa Kambi Kazi kwa kuzingatia jinsi kijana anavyoweza kuwasiliana na wenzake, nidhamu, ufahamu wa mambo mbali mbali wakati wa majadiliano na wenzake, umri na namna anavyofuata kanuni na taratibu za Kambi Kazi pamoja na kuwa na afya nzuri.

(c) Zanzibar tunapokea wageni wa Kitaifa na Kimataifa kila mwaka wakati Kambi Kazi zinapofanyika. Zanzibar tunapokea wageni kutoka Kenya, Ujerumani, Marekani, Korea, Czechoslovakia, Ireland, Sweden, Japan, Finland, Ufaransa, Austria, UK, Canada na Nertherland.

Mhe. Mwenyekiti, Mikoa ya Kaskazini Pemba na Kaskazini Unguja haijawahi kuandaa Kambi Kazi za Vijana za Kimataifa ndio maana hakuna vijana waliofaidika na Kambi Kazi hizi. Hata hivyo, Wizara inaangalia uwezekano wa kufanyika Kambi Kazi hizo katika Mikoa hiyo kwa kushirikiana na Uongozi wa Mikoa.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amezungumzia Kambi Kazi tumeelewa lakini bado nataka ufafanuzi zaidi.

(a) Je, Kambi Kazi hizi kwa hapa petu hufanyika katika maeneo gani?

(b) Je, gharama za kambi hizi wanagharamia nani kwa wageni na hawa wenyeji?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, Kambi Kazi hizi zinafanywa na Uongozi wa Mikoa na wao ndio wanaogharamia.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, katika swali mama la Mhe. Ali Abdalla Ali alitaja neno UVIKIUTA, naomba Mhe. Waziri anipe maana ya neno hili.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, UVIKIUTA ni kifupisho, ni Umoja wa Vijana wa Kambi Kazi Tanzania. Ninaamini kwamba si mara ya kwanza hili neno kutokezea. Kwa hivyo, kwa kuwa Mhe. Mwakilishi na yeye ana vijana alikuwa anapaswa alijue. Kambi Kazi hizi zikiongozwa kwa mashirikiano na huyu UVIKIUTA tumeshazifanya hata kule Pemba. Sasa anatakiwa ajue masuala kama haya kwa vile anao vijana katika jimbo lake.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuhakikisha kwamba vijana wetu wanawekwa katika makambi maalum kwa ajili ya kuitangaza nchi yetu. Lakini pia kuleta uhusiano mwema kati yetu na nchi hizo ambazo amezitaja Mhe. Waziri. Ninaamini jambo kubwa linalotakiwa hapa ni ushirikiano na kupata mambo mbali mbali ya maendeleo.

Je, pamoja na faida iliyopatikana ya vijana wetu kutembelea katika nchi mbali mbali alizozitaja Mhe. Waziri. Kuna faida kubwa nyengine ipi inayopatikana ya misaada au mambo mengineyo kwa ajili ya vijana wetu ambao wapo hapa na watahitajika kwenda huko?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ziko faida nyingi zinazopatikana. Kwanza katika kushiriki ile Kambi Kazi yenyewe unajifunza mashirikiano, unajifunza uhusiano mwema, unajifunza hata lugha na unajifunza kuwajibika katika shughuli za kijamii, jambo ambalo lina umuhimu. Sasa unapotoka nje unajifunza mengi zaidi kwa sababu kusafiri nako pia ni kujifunza, na mara nyengine itabidi ujifunze lugha, uwasiliane kwa lugha na unapotoka kule ukaja hapa pia unakuwa na mwamko mwengine. Kwa hivyo, hata wale vijana wenzako unaoshirikiana nao unaweza

kuwatilia ile elimu uliyoipata ndio manufaa yenyewe yanayopatikana katika shughuli kama hizi.

TAARIFA

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nina taarifa ya masikitiko kwamba Mhe. Waziri amelipotosha Baraza. Kwa sababu tafsiri ya UVIKIUTA alivyoitoa sivyo. UVIKIUTA ninavyofahamu mimi ni Umoja wa Vijana wa Kikristo Tanzania na kwa Kiingereza huitwa *Youngmen Christian Organization (YMCA).*

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa taarifa. Sasa kama taarifa imepatikana kwa nini nakuja kuulizwa mimi swali hapa kama mtu ana hakika nalo hilo jambo.

Mhe. Mwenyekiti: Swali kauliza Mhe. Said Ali Mbarouk, Mhe. Haji Faki Shaali amesaidia. Sasa hiyo tafsiri yake ni sawa aliyoisema?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako mimi sikuja hapa kubishana, mimi nimekuja hapa kuweka mambo sawa. Mimi ninachojua mambo ya vijana, sasa kama anayo taarifa nyengine mimi nitashukuru sana anielimishe. Kwa sababu mimi sio *hundred percent,* wala mimi sio Mungu, mimi niko hapa kwa sababu ya kuendeleza maendeleo ya vijana, wanawake na watoto. Sasa kwenda kwenye nahau hiyo mimi si shughuli yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri uliposema UVIKIUTA uliitafsiri vipi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi tafsiri yangu ndio hiyo niliyosema na sirudii tena nimemaliza hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri rudia tafsiri uliyosema.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilivyodhani tuna mambo ya msingi sana ya kuyajadili katika muda wetu muhimu na adhimu wa maendeleo ya vijana wetu. Sikutegemea kwamba tutakuja hapa tubishane *abbreviation,* hilo haliniridhishi hata kidogo. Mimi nafikiri nafasi hii ni adhimu na ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Taifa letu hapa, lakini tukija kufanya hapa Baraza la Kiswahili hapa si pahala pake. Sasa ninavyojua mimi Umoja wa Vijana wa Kambi za Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, UVIKIUTA ni Umoja wa Vijana wa Kambi za Kimataifa, hiyo ndio tafsiri anayoijua Waziri. Sasa wanaotaka kusema UVIKIUTA ni Umoja wa Kikristo waamini hivyo, wanaotaka kusema Umoja wa Vijana wa Kambi za Kimataifa waamini hivyo.

Nam. 27

Utoaji wa Mikopo ya Kuwawezesha Wananchi

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Mpango wa Serikali kuhusu mkopo wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na biashara tayari zoezi hili limeanza Kisiwani Pemba na hadi kufikia mwezi Septemba, 2009 kwa upande wa Mkoa wa Kusini Pemba benki imeshatoa mikopo kwa watu 66 yenye thamani ya Tsh. 185 milioni kati ya hizo Tsh. 151 milioni zimetolewa kwa Wilaya ya Chake Chake na Tsh. 33.7 milioni zimetolewa kwa Wilaya ya Mkoani na Mkoa wa Kaskazini Pemba watu 11 wamepata mikopo yenye thamani ya Tsh. 24.9 milioni kati ya hizi Wilaya ya Wete imepata Tsh. 13.5 milioni na Wilaya ya Micheweni Tsh. 11.4 milioni.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni tofauti ya utoaji wa fedha ni kubwa kati ya Wilaya na Wilaya ni vigezo gani hutumika kutoa mikopo hiyo?
(b) Tunasikia vikundi vya walemavu na maalbino wao hawamo katika mkopo wa mfuko huu. Je, ni kweli suala hilo?
(c) Vikundi vingi na watu baadhi yao hukosa mkopo huambiwa hawana sifa na hawakopesheki. Je, ni sifa gani hizo?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

Tofauti ya utoaji wa fedha za mikopo ni kubwa na ipo kati ya Wilaya na Wilaya. Hii inatokana na kwamba baadhi ya waombaji wanatofautiana katika kukamilisha sifa na vigezo vilivyowekwa. Sifa na vigezo vyenyewe ni kama ifuatavyo:-

(a) Muombaji awe na:
    i. Umri wa miaka 18 na zaidi.
    ii. Mkaazi na awe na kitambulisho cha Mzanzibari.
    iii. Mradi wa kuombea mkopo na kuonesha mchanganuo wa biashara yake au mradi.

iv. Kujaza fomu ya kuombea mkopo ambayo hupatikana kwa Sheha wa Shehia husika kwa kuongozwa na kukaguliwa na Kamati ya Uratibu ya Wilaya. Benki ya Watu wa Zanzibar hufuatilia kwa kina miradi iliyoombewa mikopo na huwapatia mikopo hiyo wenye kutimiza hayo yote kwa mujibu wa miradi yao.

(b) Si kweli kabisa kwamba vikundi vya Walemavu na Maalbino kuwa hawamo au hawahusiki na mikopo yenye masharti nafuu na uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwani hawa ni miongoni mwa wananchi wa Zanzibar pia. *Almuradi* cha msingi ni kufuata utaratibu wa kuomba ipasavyo. Wajasiriamali wanapatikana ndani ya vikundi na watu wenye Ulemavu na Maalbino wamo pia wameweza kunufaika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amekiri kwamba vikundi vya Walemavu na Maalbino wanapata mikopo. Je, tangu kutoka mikopo hii ni vikundi vingapi tayari wameshapewa mikopo hiyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu swali lake linahitaji takwimu na kwa hiyo halikuwemo katika swali mama, sasa hivi siwezi nikawa narusha maneno hapa. Kwa hivyo, nitampatia baadae na kama anataka *details* inabidi aliainishe kwenye swali lake la msingi.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Katika hoja ya msingi Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali aliulizia kuhusu tofauti kubwa ya Wilaya na Wilaya. Lakini sio kama kaona yeye tu, hata sisi tulipokuwa tunazungumza bajeti tuliona ipo tofauti kubwa na Mhe. Waziri Kiongozi akachukua nafasi ya kukinga kifua akasema anataka kuhakikisha kwamba wahusika wa ukopeshaji warejee katika maeneo ambayo walipita na mikopo ikawa kidogo, hasa ulipoonekana Mkoa wa Kaskazini mzima umepata milioni 6.

Je, Mhe. Waziri kwa ile kauli ya Mhe. Waziri Kiongozi na juhudi za Wizara pamoja na shughuli zinazofanywa na Wilaya, Mkoa wa Kaskazini umefanikiwa kuongeza kiasi gani kutoka milioni 6 hadi sasa. Naomba nijue katika Wilaya ya Kaskazini ‘A’ ina kiwango gani cha mikopo hadi sasa?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyoelezana hapa kwamba upatikanaji wa mkopo pia

unaendana na wale watu ambao watawasaidia wananchi ili wajaze zile fomu sawa sawa na zisikwame.

Kwa hivyo, mimi kwa sasa hivi sina hiyo *breakdown* ya hizo pesa zilizopatikana Mkoa wa Kaskazini. Lakini mwenyewe Mhe. Mwenyekiti, kama ametia jitihada na kufuatilia atakuwa anajua yeye kwa sasa hivi watu wangapi wamepata kule Kaskazini.

Nam. 41

Uimarishaji wa Afisi ya Wizara ya Wanawake – Pemba

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Pemba ina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba malengo na shughuli za Wizara yanatekelezwa kama yalivyopangwa. Hata hivyo, Wizara hii kwa upande wa Pemba bado inakabiliwa na tatizo kubwa la Jengo la Afisi kuwa dogo na kupelekea shughuli za wizara kutekelezwa katika hali ya kujifinya. Aidha, Wizara inakabiliwa na uhaba mkubwa wa vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri na kusababisha usumbufu katika utekelezaji wa kazi za Wizara.

(a) Huko nyuma kulikuwa na mpango wa kujengwa Jengo la Afisi ya Wizara hii kwa mashirikiano na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji Pemba, mpango huo umefikia wapi?

(b) Kwa kuwa vitendea kazi vikiwemo vile vya usafiri ni suala muhimu katika utekelezaji wa kazi za kila siku. Je, Wizara ina mpango gani na suala hili?

(c) Suala la Elimu kwa Wafanyakazi nalo lina umuhimu wake katika utekelezaji wa kazi. Je, ni wafanyakazi wangapi mpaka hivi sasa kwa upande wa Pemba wamekwishapatiwa mafunzo mbali mbali?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lakel Nam. 41 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba huko nyuma kulikuwa na mpango wa kujenga Jengo la Afisi ya Wizara hii kwa mashirikiano na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji Pemba. Kwa sasa mpango huo wa

kujenga pamoja haupo tena kutokana na kwamba baada ya ukaguzi kufanyika imeonekana kwamba kiwanja hicho ni kidogo hakitoweza kujengwa jengo litakaloweza kuchukua Wizara mbili. Kwa hali hiyo, Wizara yangu imefanya mawasiliano tena na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kupatiwa eneo jengine ambalo litaweza kujengwa jengo la Afisi ya Wizara huko Pemba. Kwa kuwa Mhe. Waziri wa Wizara hiyo yuko hapa naamini akiondoka hapa tu atakwenda kuamrisha nipewe hicho kiwanja haraka sana.

(b) Ni kweli kwamba vitendea kazi vikiwemo vile vya usafiri ni suala muhimu katika utekelezaji wa kazi za kila siku. Wizara yangu inalielewa hilo na moja kati ya mikakati inayochukuliwa na Wizara ni kwamba panapotokea fursa ya kupatikana vyombo vya usafiri huzingatia hali halisi ya mahitaji kwa Unguja na Pemba.

(c) Kwa mwaka 2008/2009 Wizara yangu ilisomesha jumla ya wafanyakazi 21, kati ya hao 15 kutoka Unguja na 6 kutoka Pemba. Kulingana na hali ya Bajeti ya Wizara yenyewe, utaratibu uliopo ni kwamba mfanyakazi achangie baadhi ya gharama na Wizara itasaidia pale palipobaki. Hivyo, wafanyakazi hao ndio waliomudu kufanya hivyo.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, vitendea kazi hasa usafiri ni muhimu sana katika ufuatiliaji wa shughuli za kila siku. Wizara hii inagusa maeneo muhimu hasa shughuli za wanawake na vijana.

Je, kwa kuwa haupo, Mhe. Waziri ameandaa utaratibu gani wa nauli kwa Maafisa wetu kuweza kuwapatia pesa wapande gari ili wawafikie wananchi wetu kwa kutoa huduma. Kwa sababu sasa hivi *Alhamdulillah* Unguja na Pemba usafiri upo wa gari za daladala na nyenginezo?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi kwa hali ya fedha kwa ajili ya matumizi ya wizara hii. Tungependa sana tuwe na fedha za kutosha kufanya yale ambayo ya muhimu lakini bajeti yetu inakuwa finyu na tunaipitisha hapa hapa. Kwa hivyo, endapo Baraza hili litakapoona umuhimu wa kutupatia pesa za kutosha, basi tutaweza kujipanga, tupate vyombo na tuwapatie wafanyakazi nauli. Lakini sasa hivi hali yetu sio nzuri naomba nikiri hadharani.

Nam. 10

Elimu kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha kutolewa kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi

Mhe. Ame Ussi Juma – Aliuliza:-

Pamoja na ukweli kwamba Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na inatekeleza majukumu yake kwa msingi wa Ibara ndogo ya (2) ya Ibara hii, Wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wawakilishi wa wananchi, hawaijui ama hawaifahamu namna inavyotekeleza majukumu yake.

(a) Je, Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kufanywa semina kwa Wajumbe wa Baraza hili ili waweze kujua kwa kina utekelezaji wa majukumu ya Tume hii?

(b) Kwa kuwa Tume hii ni ya Muungano. Je, inawakilishwa na wajumbe wangapi Wazanzibari?

(c) Je, kuna changamoto zipi zinazoikabili Tumehii katika utekelezaji wa majukumu yake?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, nakiri kwamba ni kweli kuna umuhimu mkubwa wa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakapata semina ili wawe na uelewa wa kutosha juu ya kazi na majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha. Uelewa wao ni imani yangu kwamba utawarahisishia katika kuchangia na kuzishauri serikali zetu mbili katika kuchangia juu ya kero mbali mbali zinazoukabili Muungano wetu, hususan kwa upande wa masuala ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba juhudi kubwa zinaendelea kufanyika kwa Tume kuweza kukutana na Baraza lako tukufu na kwa kuanzia Tume inatarajiwa kukutana na Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na

Mashirika ya Umma *(PAC)* na ile ya Fedha na Uchumi hivi karibuni katika tarehe muafaka.

(b) Kwa mujibu wa Sheria Tume ina Wajumbe 7 walioteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati yao watatu wanatoka Zanzibar na kati ya hao watatu wanaotoka Zanzibar basi mmoja amekuwa Makamo Mwenyekiti wa Tume hiyo. Kwa hiyo, Tume ina jumla ya Wajumbe 7.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na changamoto zinazoikabili Tume, changamoto hizo zinaweza kugawika makundi matatu.

(i) Upya wa Tume,
(ii) Ushughulikiaji wa Mapendekezo ya Tume
(iii) Masuala ya Sheria.

Kuhusu upya wa Tume, wakati wa kuanzishwa kwake kazi mwaka 2003 ililazimika kujijenga kitaasisi kwa kuandaa mapendekezo ya muundo *(organization structure)* kama *establishment*, ajira pamoja na kuweka taratibu za ndani za uendeshaji. Masuala yote haya ni muhimu kwa taasisi mpya na yanahitaji kuidhinishwa na ngazi mbali mbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yanachukua muda hadi kukamilika kwake. Mengi ya masuala haya kwa sasa yameshapatiwa ufumbuzi baada ya kusuasua kwa muda mrefu.

Kuhusu ushughulikiaji wa mapendekezo ya Tume, changamoto ni kuwa hapo kabla hakukuwa na utaratibu baina ya Serikali zetu mbili wa namna ya kushughulikia mapendekezo hayo kadri yanavyopokelewa. Kwa sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeshakubaliana, kwamba kila upande uyapitie mapendekezo hayo, kuyapitisha katika ngazi za serikali na hatimaye kuwasilisha katika kikao cha kutatua kero za Muungano, kilicho chini ya Uwenyekiti wa Mhe. Makamo wa Rais kwa mjadala wa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya sheria ilibainika baada ya tume kuanza kazi rasmi. Mapendekezo ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza yaliwasilishwa katika serikali zote mbili kwa kupata maoni kabla ya kuwasilishwa katika vyombo vyetu vya kutunga sheria.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kurejea tena kwamba nyingi ya changamoto hizi zimetokana na upya wa tume, ambayo imeteuliwa kwa mara ya kwanza katika historia ya Muungano wetu mwezi Machi, mwaka 2003, ahsante.

Mhe. Ame Ussi Juma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alikubali kwamba ipo haja wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kufanyiwa semina.

Je, anaweza kutuambia ni lini semina hiyo itapangwa ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokubali kwamba hili ni suala muhimu na tutaandaa utaratibu semina hii utapangwa. Najua hizi siku mbili au tatu hapa na kama *weekend* hii iliyopita tulikuwa na semina ya wajumbe wako Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya PAC na Kamati ya Fedha. Kwa hivyo, sisi Wizara ya Fedha tukisema tunatenda. Kwa hivyo, nakuahidi tupe nafasi tutapanga na tutatekeleza.

Mhe. Mwenyekiti: Semina hii Mhe. Waziri iwe, maana ni jambo zito hili.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nikupongeze wewe Mwenyekiti, kwa kuniulizia lile swali la kwanza ambalo nilikuwa nataka kumwambia Mhe. Waziri. Kwa kuwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wana haki ya kujua hii tume na mwenendo wake na kwa kuwa tume hii ni ya Muungano na hakuna kamati moja ambayo inahusika peke yake isipokuwa Baraza zima kwa niaba ya wananchi. Pamoja na juhudi hiyo ya kusema kwamba kulikuwa na semina ya wajumbe wa Kamati ya PAC na kamati ya Fedha na Uchumi.

(a) Je, Mhe. Waziri haoni hilo ni kosa na baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakosa haki hiyo ya kujua ?

(b) Hivyo Mhe. Waziri atanieleza nini kamati hii au tume hii imeundwa mwaka 1977 na imeanza kazi mwaka 2003 katika makati hiyo mpya. Je, hivi haoni miaka hiyo ni mingi na kero ambazo ziko kukosa haki zetu katika tume hiyo hazipatikani kisahihi ili wananchi wote tufaidike?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kabla hujajibu. Mhe. Mjumbe suala la kamati mbili alikuwa anaonesha kuwa wao wakisema wanafanya, ndio ilikuwa maana yake pale, kwa kuwa ameshafanya semina kama hiyo na semina kubwa kafanya. Mimi naamini na hii ya watu wote atafanya. Hili nafikiri umeshasema wazi, atafanya Mhe. Mwinyihaji siku hizi *Alhamdulillah* tusiwe na wasi wasi naye.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kuhusu muda mwingi kwa tume hii tokea ilipoanza kazi. Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Ali Suleiman Ali alivyouliza. Ni kweli kwamba tume imeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 134 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1997 na sheria ya tume ya pamoja ya fedha sura ya 140 imeanzishwa mwaka 2003.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema matatizo makubwa wakati ule niseme tu kuwa ilianzishwa tu kama jina, lakini hakukuwa na vyombo vya kufanyia kazi, walikuwa hawana meno. Mfano, sio afisi tu, hata zile taratibu za kuifanyia kazi hazikuwepo, ndio nikatumia neno lile walikuwa wanasua sua tu kama wanapigwa mpira, wakienda huku na huku mpaka hivyo vyombo sasa Mhe. Rais akavihalalisha na akatoa maelezo yakakubalika ndio wakaanza kazi rasmi.

Kwa hivyo, ni hatua kubwa sana kwa kweli tume hii imeshafanya pamoja na kutoa mapendekezo ya tume kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchambua gharama za Muungano. Nafikiri Waheshimiwa Wajumbe tulipata, sijui kama tulipata *copy* hii. Maelezo yalitolewa ya msingi, nafikiri yako serikalini kwanza huku hayajafika bado. Sasa serikalini tunayajadili na tunayazungumza, tukimaliza kama nilivyosema tutakuja kufanya semina Baraza la Wawakilishi, tuwapeni hasa yale mambo ya msingi na mtushauri ipasavyo, basi turudi tukaamuwe serikalini na kukubaliana na wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu sasa umeshawekwa na hizi changamoto zote zimeshajitokeza na tumeshazitambua tuko kwenye mtiririko. Siku zote huwa nasema suala hili ni zito, linahitaji ustahamilivu wetu, uadilifu wetu na umoja wetu. Tusiamuwe tu kwa papara papara, haya ni mambo ya msingi kabisa. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Ali Suleiman Ali na Waheshimiwa Wajumbe wengine muzidi kutuvumilia, naamini tunakaribia mfundani, na siku zote mfundani ndio pazito sana.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kama nimesikia vizuri kwamba si muda mrefu kamati ya fedha na uchumi pamoja na kamati ya mahesabu ya serikali atakutana nayo. Lakini kidogo nimepata mshtuko.

Kamati ya Fedha na Uchumi kazi zake ni kuelekeza na kuangalia namna ya njia za vianzio vya mapato pamoja na mambo mengine na kamati ya *PAC* kazi yake ni kuipitia na kuifanyia kazi ripoti ya Mdhibiti Mkuu wa mahesabu ya serikali.

Naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kipindi hicho kidogo kinachotarajiwa kukutana na Mhe. Waziri na kamati hizo, zikafanye kazi gani au zipate maelezo gani wakati tume hii haijafanya kazi hapa Zanzibar na haina mahesabu ambayo inataka kuchunguzwa ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hizi ndio tume zetu mbili zinazoshughulika na mambo ya fedha hapa. Kama alivyosema Mhe. Mjumbe mwenyewe kwamba ile kamati ya Fedha na Uchumi kazi yake inashughulika na uchumi na mambo ya fedha, na hii ya *PAC* inashughulika na uchunguzi wa hesabu za mambo ya fedha.

Kwa hivyo, ni imani yetu kwamba watasaidia kutupa ushauri. Lazima tukumbuke kwamba ni nini madhumuni makubwa ya tume hii, naomba nikusomee. Madhumuni makubwa ya tume hii ni:

1) kuchambua mapato na matumizi yanayotokana au yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa serikali mbili, kuhusu mchango na mgao wa kila mmoja wapo kwa serikali hizo.

2) kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya serikali zetu mbili.

3) kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano ataipatia tume na kama Rais atakavyoagiza na kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu Mhe. Ame Mati na wajumbe wengine kwamba katika kero zetu kubwa sana tulizonazo zinahusu mambo ya fedha na mapato na ugawanaji wake. Kwa hivyo, naamini Mhe. Ame Mati na nakuomba, ukiwa wewe ni mjumbe wa tume hii au hata kama ukiwa si mjumbe, lakini tutakuja kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti, kwenye semina ya Baraza tutasaidiana mawazo kwa kufikia hii azma yetu, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita Mhe. Haji Mkema Haji, labda tuelewane, baada ya Mhe. Haji Mkema kumaliza nitamwita Mhe. Waziri kuja kufanya majumuisho. Kwa hivyo, wajumbe msiwe mbali, tunataka saa 6:00 au 7:00 tukale wali.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunikumbuka ili niweze kumalizia mchango wangu ambao nimeanzia jana, unaohusiana na mswada huu wa sheria ya fedha chafu.

Mhe Mwenyekiti, nilimalizia jana kwamba Mhe. Waziri anitoe wasi wasi kwa sababu hakutuorodheshea yale mambo kwa kutuwekea bayana kwa wananchi juu ya neno fedha chafu.

Majuzi tulikuwa na mswada hapa wa madawa ya kulevya. Namshukuru Mhe. Waziri wa Afya aliweza kuorodhesha maeneo yote ya madawa ya kulevya saikotropiki, petrotic na *cocaine*. Lakini mpaka tunachangia mswada huu, nina hakika bado wajumbe hawajajua maeneo kamili au orodha ya pesa chafu ziko vipi. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri atuwekee bayana ili mtu wa kawaida, kwa sababu sheria hii haitafanyiwa kazi tu wanasheria au Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Sheria hii ni ya wenyewe wananchi huko na itafanyiwa kazi na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, suala zima la utekelezaji sheria hii baada ya kuundwa ujue kutakuwa na kazi pevu. Kwa sababu fedha chafu kama inavyozungumzwa humu hatazifanya mtu mdogo, au mfanyabiashara mdogo. Kwa wale wapanga nyanya, mapera au machungwa basi hawa hawatakuwa na uwezo kabisa wa kufanya pesa chafu. Kwa sababu pesa chafu zinakuwa ni za kiwango cha hali ya juu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, serikali imejipangaje juu ya kupambana na fedha chafu, mbali ya hii sheria. La si hivyo sheria hii tutaipitisha leo, mwezi wa kwanza tunakuja Mhe. Rais keshautia saini, lakini katika utekelezaji wake kutakuwa na kazi pevu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, serikali imejipangaje juu ya suala zima la kupambana. Najua hii ndio itakuwa sehemu ya kuanzia, lakini je imejipangaje kwa hili. Kwanza kusiwe na muhali, kuoneana haya, kusiwe na ubinafsi wala kuoneana.

Mhe. Mwenyekiti, katika pesa chafu isijekuwa sasa hivi ndio kigezo au ndio fimbo ya kumkomoa mwengine. Mfano mtu awe anafanya jitihada zake, anafanya kafanya huko katika mazingira magumu kajitahidi huko, basi akaonekana sasa hivi katononoka ana magari na nyumba kadhaa, basi iwe huyo pesa chafu hizo tukamtia hatiani. Kwa hivyo, nasisitiza Mhe. Mwenyekiti, suala la uadilifu liwepo katika kuzingatia masuala haya ya kuhakikisha huu uhalalishaji au uharamishaji wa pesa chafu.

Lakini katika ukurasa wa 65 kifungu cha 5(a)(b)na(c). Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa tafsiri na madhumuni ya kujishughulisha na pesa chafu. Yameelezwa maeneo matatu,

Kifungu cha 5(a)(b)na(c)

(a) Ikiwa kuna deni analodaiwa mtu huyo, kufanya malipo kwa mtu yeyote kupunguza kima cha deni hilo;

(b) Kuihamisha mali hiyo kutoka Zanzibar;
(c) Kupokea au kutoa zawadi kwenye mali hiyo.

Sasa hasa katika hiki kifungu cha (c), vipi mtu anaweza kupokea zawadi kisha ikageuka kuwa hiyo ni pesa chafu. Au mtu anadaiwa kamlipa mwenziwe anaambiwa hizi ni pesa chafu. Kwa hivyo, tuseme watu wanaohukumiwa au wanaotuhumiwa kuwa na pesa chafu wasilipe madeni yao, wasitowe zawadi, wasilipie huduma. Kwa hapa mimi najiuliza ni nini sheria hii imekusudia katika kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikija tena katika ukurasa 67 kifungu cha 9(1) naomba kunukuu,

Kifungu cha (9)(1)

"Endapo kosa chini ya masharti ya kifungu hiki limetendwa na kampuni au kundi la watu, kila mtu ambaye, wakati wa utendwaji wa kosa alikuwa;

Kifungu cha (9)(1)(a)

"Mkurugenzi, Meneja au mwenye mamlaka ya kuongoza au mbia";

(b) Anajihusisha na uendeshaji wa shughuli za kampuni atasemekana ameshiriki katika kutenda kosa na atalazimika kupata adhabu iliyoelezwa aktika kifungu cha 6, kama ni mshiriki katika kosa lililotendwa bila ya ridhaa yake au aliyefumbia macho kosa lifanyike na kwamba amefanya jitihada zote kuzuia utendwaji wa kosa kama angelihitajika kufanya. Ukizingatia asili ya kazi yake kwa cheo chake na kwa mazingira yalivyo".

Mhe. Mwenyekiti, napenda kifungu hiki kiandikwe vyengine. Hii ndio tunatia mwanya wa kuja kuonea watu. Ukiwa meneja, kimefanywa kitendo halafu wewe ushirikishwe kuwa umefanya kosa hilo tutakuwa tunawaonea watu. Nafikiri hapa tufanye upelelezi kabisa ndani ya kampuni, basi anayehusika akibainika basi huyohuyo akamatwe sio Meneja.

Mhe Mwenyekiti, tunajua shughuli zetu za makampuni au uongozi wowote, kiongozi kwa muda mwingi kwa mazingira yoyote anaweza kuwa hayupo, anaumwa au amesafiri. Akatokezea mfanyakazi akafanya tendo hilo kwa makusudi labda kumuharibia sifa au kwa maslahi yake mwenyewe. Akaona kwamba sasa hivi Mhe. Haji Mkema hayupo ngoja nifanye hivi. Baadaye kwa sababu mimi ndio najulikana ndio meneja wa kampuni hiyo, halafu kifungu hiki kije kinibane basi tutakuwa tunafanya kosa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema sheria iweke wazi kuwa itafanya mbinu kuhakikisha kwenye kampuni inafanya upelelezi wa kutosha na kubaini mtu halisi aliyetenda kosa na yeye achukuliwe hatua. Kwa sababu kwa njia moja au nyengine anaweza kuwa hausiki. Lakini ukiweka wazi tu kwamba kampuni ikifanya kosa basi akamatwe meneja. Hapa tutakuwa tunakiuka sera yetu ya utawala bora. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kifungu hiki akitizame upya.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 11 katika sehemu ya tatu ya mswada huu ambacho kinazungumza, Kitengo cha Upelelezi wa Taarifa za Fedha na Kamati ya Kitaifa. Mimi sina mashaka na hicho kitengo kitasaidia. Lakini katika kifungu cha 11, naomba kunukuu.

Kifungu cha 11

> "Kutakuwa na Kamati ya Kitaifa ya kushughulikia udhibiti wa usafishaji wa fedha haramu".

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nina mchango. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amekuwa kimpya hapa kwenye kamati hii ya kitaifa ataiunda vipi, kamati hii itakuwa na watu wangapi na kamati hii itakuwa na watu wenye sifa gani. Kaeleza tu kamati, lakini amekuwa kimya. Nafikiri hapa mimi nina wazo kidogo. Kamati hii ni lazima iwe na watu mahiri kabisa na wenye utaalamu na uadilifu, ambao watakuwa na uwezo wa kufanya haki katika kufanya kazi hii.

Kwa mfano, mimi ningependekeza basi kamati hii iwe angalau na wanasheria. Mwanasheria wa kitengo cha kujitegemea mmoja, mwanasheria wa serikali, Kamishna wa polisi au mtu mwenye sifa za kuwa Jaji wa Mahakama Kuu hiyo angalau ingekuwa tume kamili.

Kwenye kipengele hiki Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu yeye Mhe. Waziri amekuwa kimya basi mimi napendekeza kamati hii iwe katika mfumo wa aina hiyo, ili uweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia katika mswada huu nije katika ukurasa wa 83, hii ni sehemu ya sita. Amri za Kulipa Faini ya Fedha. Katika kifungu cha 34(1) hapa kinazungumzia amri ya kulipa faini.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunamzungumzia mtu ambaye amebainika na fedha haramu au fedha zilizokuwa amezisafisha au kuzihalalisha. Baada ya kumuona na hatia sasa tunasema apigwe faini. Makosa haya Mhe. Mwenyekiti, yasiwe na faini. Huyu kwa njia yoyote hatakosa fedha za kulipa. Hakuna faini hata moja ambayo utamtoza akashindwa kulipa ikiwa kaweza kutengeneza mapesa chungu mzima, tuseme faini hiyo itakuwa ni kiasi gani, kwa sababu haikutajwa. Huyu aliyeingia kwenye biashara hii Mhe. Mwenyekiti, ni lazima atakuwa na uwezo na sio mtu mmoja tu, hapana. Biashara hii hafanyi mtu peke yake ni lazima kutakuwa na mtandao ambao wanakuwa wanasaidiana kwa kuwasiliana kila mara.

Mhe. Mwenyekiti, wakishasikia mwenzetu kakamatwa basi kakamatwa na nani, inakwenda mahakama gani, Jaji ni nani. Sasa wewe ukaweka kifungu cha faini basi jambo hili kwa faini, mitandao ya Kenya, Zambia, Uturuki na kwengineko mara moja zinaweza zikaletwa pesa akalipa faini na mtu bado akahisi hajatiwa adabu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwenye makosa ya aina hii faini haitakuwa dawa wala haitakuwa adhabu sahihi ambayo itaweza kumkomoa au kumtia adabu au kumrekebisha mkosa wa aina hii.

Mhe. Mwenyekiti, adhabu sahihi hapa ni kifungo tu kizito basi, mambo ya faini kwa watu kama hawa haitsaidia. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hata hiyo faini yenyewe ikilipwa itakuwa ni katika pesa hizo za haramu tunazipokea. Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika misingi hiyo miwili mimi sikubaliani nayo kuwa katika sheria hii kuwepo na adhabu za faini au mambo mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika sehemu ya saba kifungu cha 39(1) hapa kinazungumzia kugomboa mali. Hiyo ndio hatari ninayoiogopa. Sasa kama kuna kitengo cha FIU, kuna kamati hiyo ya kusafisha, mpaka mali imechukuliwa halafu tunatia kipengele cha kugomboa mali maana yake nini si ndio tunaweka ushoroba huo au *corridor* ya kuweza kutia nguvu biashara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kipengele hiki nakipinga. Mali iliyotaifishwa kusiwe na mwanya wowote tena tukaweke sheria ya kugombolewa. Labda hiyo tumuachie mamlaka Jaji ambayo kikatiba hayazuiliki. Lakini sisi tukaanza kuweka mwanya mali ambayo imeshakamatwa katika njia ya haramu, halafu tena tuweke utaratibu wa kuikomboa. Mheshimiwa mimi hili nalipinga na tutakuwa tunacheza hapa, hatufanyi kazi ya kutafuta au kuweka usawa au uhalali katika mazingira yetu ya kiuchumi pamoja na fedha.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine katika mswada huu, nitaingia katika sehemu ya tisa ya mswada katika kifungu cha 75(1)(a)(b). Uwezo wa Kufanya Upekuzi wa Waraka. Mhe. Mwenyekiti, pamewekwa utaratibu hapa lakini kwa nini tunajizonga. Kazi hizi zinafanywa na vyombo vyetu vya dola, na vina utaratibu wake kama kupekua au vyovyote, lakini wameshaweka utaratibu wao jeshi la polisi wana sheria zao na sisi tunaweka sheria nyengine, kwa nini tunajizonga.

Mhe. Spika, mimi naona kwa vipengele hivi tunaufanya huu mswada kwa makusudi kuwa mkubwa wala havitatusaidia kitu. Tutajizonga makusudi kwa kuweka vipengele ambavyo vitatoa mwanya kwa mhusika ili aweze kupenya. Vipengele vidogo vidogo kwanza vitafanya rasimu kwa kesi, pia vitatoa mwanya kwa wahalifu kuweza kutokea ikiwa havikutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, jeshi la polisi lina utaratibu wake. Lakini hapa nafikiri tumewawekea utaratibu hawa wenzetu ambao sasa hivi tuko katika utawala bora, kuna askari jamii hawa nafikiri tuwawekee utaratibu, kwa sababu kazi hii tuna hakika jeshi la polisi peke yao hawataweza. Sasa hivi kuna polisi jamii ndio wa kuwawekea utaratibu wa namna gani na wao watapambana.

Nafikiri Mhe. Mwenyekiti, tukifanya hivyo juu ya suala hili, basi mimi naamini polisi jamii wanaweza kufanya kazi vizuri zaidi kuliko hawa tulionao. Uzoefu, tuwatengee mazingira ya kisheria polisi jamii kwa sababu wao ndio walioko mitaani wanawajua wanaozunguka. Kwa hivyo, tuwaekee vipengele vizuri, ili Polisi Jamii waweze kuifanya kazi hii, na Jeshi la Polisi wapelekewe kwa hatua za kupelekwa Mahakamani au kwenye hiyo Kamati ya Kitaifa. Lakini sehemu za upekuzi pamoja na kazi nyengine za huku chini wakati wa kumgundua huyu mhalifu, basi nafasi waekewe hawa wenzetu Polisi Jamii, yaani wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, pia Vikosi vyetu vya SMZ kwa upande wa Zanzibar ambavyo havina mamlaka au sheria zile za upekuzi ambazo zinawatawala. Lakini kwa Jeshi la Polisi wanazo sheria zao ambazo zinawapa mamlaka kamili ya kufanyakazi hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya michango hiyo nina imani marekebisho pamoja na maelezo au mapendekezo ama mashauri mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe waliyoyatoa ni muhimu sana. Kwa hivyo, ni vyema yakafanyiwa kazi, ili sheria hii iweze kufanyakazi vizuri na kuepukana na janga hili la fedha haramu. Lakini tuhakikishe kwamba serikali itapambana na changamoto kubwa juu ya suala hili *(Makofi)*.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, nisije nikasahau kwenye suala hili, kwa kweli nisingependelea chombo chetu cha Mahakama kushughulikia mambo haya kama kweli tunataka kufanikiwa katika hili. Hivyo, ni bora pangekuwa na tume

yenye uwezo wa kushughulikia mambo haya. Kwa sababu, huu utakuwa na upana zaidi pamoja na *seriousness*. Kwa maana hiyo, ni vyema pawe na tume ambayo itashughulikia masuala haya, ambayo itatoa hukumu pamoja na mambo yote.

Mhe. Mwenyekiti, huo ndio ushauri wangu katika Mswada huu wa Sheria ya Udhibiti wa Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo Mengi Yanayohusiana na Hayo ya mwaka 2009, ambayo itaanza kutumika baada ya sisi kupitisha na Mhe. Rais wa Zanzibar kuweka saini.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii pamoja na moyo, kwa sababu nilikuwa sitaki, lakini kwa kunipa nafasi hii umenitia moyo, ili niweze kusoma huu mswada na mimi nipate ya kuweza kuchangia kwa ajili ya kuboresha mswada huu.

Baada ya hayo mimi mwenyewe binafsi, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Koani naunga mkono, baada ya Mhe. Waziri kuifikiria michango yetu, ili sheria hii tuweze kuitumia *(Makofi).*

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwa kunikubalia na kunipatia wasaa huu wa kuja kufanya majumuisho ya hoja zao mbali mbali, walizochangia au waliotuuliza pamoja na zile walizotoa fikra za kuendeleza mswada wetu huu wa Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, lazima nikiri kwamba michango tumeipokea mingi sana na takriban Waheshimiwa Wajumbe wapato 20 wamechangia. Kwa kweli kama nilivyosema michango mizuri ambayo ni mingi na nitajitahidi kwa muda mchache tu au kiasi, kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa hoja hizo.

Mhe. Spika, kwa ujumla Waheshimiwa Wajumbe wengi sana wamejikita kwenye maeneo kama tisa hivi, ambayo tumeyaorodhesha. Kwanza Waheshimiwa Wajumbe wengi wamejikita katika suala la utekelezaji wa sheria na usimamizi wake na kuwa na wasi wasi kwamba tunapanga vizuri tena sheria ni nzuri je utekelezaji wake tutauweza?

Kwa hivyo, ninawaahidi Mhe. Mwenyekiti kama tulivyoona hata Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na sisi wenyewe tulivyoona tatizo la janga la madawa ya kulevya linavyoanzia, tukakubali kwamba tutasaidiana kulifanyia

kazi. Kwa maana hiyo, katika suala hili serikali itasimama kidete kwa kushirikiana na nyinyi, ili tuone kwamba tunalipatia ufumbuzi au kulidhibiti lisishamiri nchi mwetu *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili Waheshimiwa Wajumbe waliyoitoa kwamba watoa taarifa walindwe pamoja na kupewa zawadi, japo Mhe. Haji Mkema Haji muda si mrefu alisema pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine, kuwa zawadi hizo tulinganishe ni zawadi gani na tuzi-*qualify* ipasavyo.

Tatu muundo wa Kamati ya Kitaifa pamoja na Kitengo cha *Financial Intelligence Unit*, nacho Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia hasa muundo wake na vipi tumechukua vile vifungu vya sheria ile ya Bara. Kwa hiyo, nitayatolea maelezo yote hayo.

Suala la nne Mhe. Spika, ilikuwa ni michezo ya kamari pamoja na bahati na sibu. Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia masuala hayo na walitaka kujua kwamba vipi tutayaainisha na hasa kwa maadili yetu hapa Zanzibar ya Kiislamu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la tano ni adhabu kwa waliotiwa hatiani. Nadhani hapa kidogo tulitofautiana kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wengine walisema adhabu zilizowekwa ni nzuri, tena kubwa na zinastahiki, lakini wenigne walisema adhabu hizi ni kidogo na tuziongeze na ziwe kali zaidi, yaani watu wasikaribie huko.

Kwa hviyo, sisi kwa kuanzia tunadhani na kwa kushirikiana na wanasheria wenyewe ambao ni wataalamu hizi adhabu zilizopo kwa kuanzia tunadhani zinafaa na zitasaidia kuidhibiti hali isiendelee.

Vile vile kulikuwa na suala la sita kuhusu mafunzo na taaluma kwa wananchi wetu pamoja na taasisi husika limetiliza mkazo sana. Kwa kweli suala hili Waheshimiwa Wajumbe wengi sana wamelizungumza umuhimu wake. Kwa hivyo, sisi tumekubali kama wizara na serikali kwa jumla suala hili la mafunzo tutajitahidi kutoa mafunzo kupitia vyombo vyetu vya habari, pia semina, warsha, ili ndugu zetu, watoto wetu, pamoja na watu wote kwa jumla wajue umuhimu wa suala hili na jinsi ya kuliepuka.

Suala la saba ni kuhusu uadilifu, na ukweli kwamba tuwe waadilifu na wakweli katika utekelezaji wa suala hili, na tusimame kidete kuona kwamba sheria zinafuatwa ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hayo ni maelekezo mazuri waliyotupa na hasa wasimamizi wa sheria, yaani vile vyombo vya usimamizi wa sheria vikiwemo Polisi na *CID* na vyenginevyo. Hivyo suala hilo nalo tumelichukua.

Lakini suala zima la vitendea kazi kwa taasisi husika ambalo ni jambo la nane nalo limetiliwa mkazo, Mhe. Mwenyekiti, na hili tumelisikia. Kwa hivyo, tutajitahidi kuhakikisha kwamba kweli wale wanaohusika na masuala haya wanavyo vitendea kazi, kwa ajili ya kuwasaidia katika utekelezaji wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti suala la tisa ambalo limezungumzwa sana kufanywa kwa utafiti kwa matumizi ya sheria nalo hili tumelipokea na tutalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti kwa ujmla kama nilivyosema kulikuwa na michango ya Waheshimiwa Wajumbe 20. Sasa naomba niwatambue na kuwashukuru sana kwa kazi yao nzuri.

Lakini kabla sijawataja Mhe. Mwenyekiti kwa mara nyengine tena naomba nitoe shukurani zetu za dhati kabisa kwa Kamati ya Fedha na Uchumi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kamati kama nilivyosema wakati nilipokuwa nikiwasilisha imefanyakazi nzuri sana kwa kushirikiana na wataalamu wetu tumepitia mswada huu neno kwa neno na kifungu na kifungu na kurekebisha mpaka tukapata hii sura mpya ya mswada.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya Waheshimiwa Wajumbe wengine walipokuwa wakichangia walikuwa wakirejea ule wa zamani ambao nilisema tuuache. Kwa hivyo, nafikiri baada ya kupata huu mpya wataona nakumbuka kama Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja alisema hoja zake nyingi sana zimeshajibiwa baada ya kuona huu mswada mpya. Hivyo, tunawashukuru sana kamati ile kupitia Mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwa kweli kazi waliyoifanya ni nzuri sana na wajumbe wote *(Makofi)*.

Vile vile kwa upande wa Wajumbe wengine waliopata kuchangia hapa ukumbini wamejitahidi kupitia hapa na pale.

Mhe. Rashid Seif Suleiman aliniambia nilipoiwasilisha huu mswada nilikuwa *very brief*. Mhe. Mwenyekiti, nilihisi sina maelezo mengi zaidi, kwa sababu mambo mengi yameshawekwa kwa ufasaha na yako wazi, sasa nikaona niwache wazi *room* sasa Waheshimiwa Wajumbe wachangie na wala sikuwa na lengo kwamba nianze kusoma yale yale niyarejee. Lakini nilihisi ile haja yenyewe imeshakidhiwa *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, niwatambue waliochangia kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi)
1. Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli wa Fedha na Uchumi)

2. Mhe. Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi
5. Mhe. Rashid Seif Suleiman
6. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
7. Mhe. Ali Denge Makame
8. Mhe. Ame Mati Wadi
9. Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi
10. Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii
11. Mhe. Asha Moh'd Hilali
12. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum
13. Mhe. Hasnuu Moh'd Haji
14. Mhe. Bihind Hamad Khamis
15. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba
16. Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira
17. Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto
18. Mhe. Abdalla Juma Abdalla na
19. Mhe. Haji Mkema Haji.

Mhe. Mwenyekiti, wote hawa tunawashukuru sana na ninaamini kama tuungekuwa na muda zaidi, basi Waheshimiwa Wajumbe wengi wangetaka kuchangia. Lakini nafikiri kama nilivyosema na wewe Mhe. Mwenyekiti umeona kwamba hoja zilikuwa zinajirejea zile kwa zile *(Makofi)*.

Jambo jengine kuhusu wale Waheshimiwa Wajumbe ambao hawakupata ile karatasi ya mswada wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo tulitoa *photocopies* na tulisambaza ya ile Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu wa Tanzania Bara wa Lugha ya Kiingereza, yaani *pages* kama nne tu. Kwa hivyo, kwa wale ambao hawajaiipata ni vyema wakaipata kwani itaweza kusaidia sana maelezo yangu pamoja na suala zima la sheria yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru kwa kuanzia Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi) kama nilivyosema kwa kazi yao nzuri. Lakini hasa namshukuru sana kwa kuona yale mapungufu yaliomo kwenye Kamati ya Kitaifa pamoja na zile kazi za Kitengo cha *Financial Intelligence Unit*. Hivyo, ushauri wao ni kwamba kwa kweli kama Zanzibar hatukuwakilishwa ipasavyo na itabidi lazima kama Zanzibar na sisi tuweze kuwemo katika kitengo hiki, ili kazi zetu ziende pamoja.

Ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti ni kuwa na hili hata Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli wa Fedha na Uchumi) alilizungumza sana, kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika jaduweli la kwanza ibara ya nne ya Katiba imeorodhesha Mambo ya Muungano. Udhibiti na Usafishaji wa Fedha

Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu na Yanayohusiana na Hayo si miongoni mwa Mambo ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, wataalamu wetu wa sheria wa pande zote mbili walikubalia kwamba suala hili si la Muungano, yaani wataalamu wetu walikaa wakakubaliana hivyo pande zote mbili. Hivyo ni vyema sheria ikawepo kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara na ishirikiane katika *Financial Intelligence Unit* na Kamati ya Kitaifa, yaani pambe zote mbili tushirikiane. Kwa sababu haya mambo huwezi kuyazuia tu hasa nchi zetu zilivyo ni vigumu sana.

Kwa hivyo, kuna Kamati ya Kitaifa nafikiri *composition* yake utaona kwenye ile karatasi ambayo tumeisambaza kwenye sheria ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mwenyekiti naomba ninukuu kifungu cha 8.

Kifungu cha 8 (1) na (2) vinasema hivi:-

1. "*There is a established of the purposes of this Act, a National Multi Disciplinary Committee on Anti- Money Laundering"*
2. *The National Committee shall be composed of -*
   - *(a) One Representative of the Bank of Tanzania, who shall be a Chairman;*
   - *(b) One Representative of the Ministry of Finance;*
   - *(c) One Representative of the Ministry of The Revolutionary Government of Zanzibar;*
   - *(d) One Representative of Attorney-General's Chambers;*
   - *(e) One Representative of Attorney-General's Chambers of the Revolutionary Government of Zanzibar;*
   - *(f) Two Representatives of the Directorate of Criminal Investigation, one of whow shall come from its office in Tanzania Zanzibar;*
   - *(g) One Representative of the Minstry Responsible for Foreign Affairs;*
   - *(h) The Commissioner of the FIU;*
   - *(i) One Representative of the Capital Markets and Securities Authority; and*
   - (j) *One Representative of the Tanzania Intelligence and Security Service".*

Mhe. Mwenyekiti, huo ndio muundo wa Kamati ya Kitaifa na kama nilivyosema utaona na sisi Zanzibar tumehusishwa kwa hili tunashukuru,

kwamba tunakwenda vizuri kabisa na watu wetu wanashiriki, tunajadiliana na kuzungumza kwa pamoja.

Hata hivyo, ukizingatia utekelezaji wa makosa ya jinai, mashtaka hufanywa pale linapotendeka kosa. Hivyo, kuna tofauti ya sheria baina ya Tanzania Bara na yetu ya Zanzibar, haiwezekani kumti hatiani mtu Zanzibar, na kushtakiwa Tanzania Bara *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile udhibiti na usafishaji wa fedha haramu sio suala la Muungano na hili nasisitiza na ndio sababu kipengele cha 10 (1) na (2) vikahitajika katika sheria hii, ili kuridhiwa na Baraza lako tukufu. Kwa maana hiyo, tumeona hakuna haja ya kutunga vyengine hivi vinakidhi haja, lakini tumeona tuvilete hapa kwa ajili ya kuridhiwa, huo ndio utaratibu unavyozungumza kwa masuala si ya Muungano. Kwa hivyo, naamini Waheshimiwa Wajumbe mtaridhia baada ya kuona hiki kiambatanisho tulivyokisambaza.

Kuhusu uanzishwa wa *Financial Intelligence Unit (FIU)* na Kamati ya Kitaifa. Kifungu cha 8 cha Sheria ya Tanzania Bara ya Kudhibiti Fedha Haramu kimeelezwa juu ya uanzishwaji wa muundo wa Kamati ya Kitaifa, kama nilivyosema ya usimamizi wa fedha haramu. Mhe. Mwenyekiti, nakla ya kifungu hicho kama nilivyosema tumesambaza kwa Waheshimiwa Wajumbe wote kama ambavyo Baraza lako litakavyoona.

Zanzibar imewakilishwa ipasavyo katika kamati hiyo kwa kuwa na wajumbe watatu kati ya 11. Kamati hiyo inayohusika pia wajumbe kutoka Taasisi za Muungano kama vile Benki Kuu, Idara ya Usalama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa *Financial Intelligence Unit (FIU)*, naomba kuahidi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama mlivyotushauri hasa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwamba tulifuatilie kwa karibu sana. Kwa kweli suala hili tunahakikisha kuwa muundo pamoja na mjumuiko wa wafanyakazi wake utakuwa na sura kamili ya Muungano kwa kuwa na watendaji kutoka Tanzania Bara na pia wa Zanzibar.

Vile vile kulikuwa na suala jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe wengi walilichangia kuhusu kupekuliwa bila ya kuwa na nguo watuhumiwa. Kwa kweli nadhani limezua mjadala kidogo. Kwa hivyo, ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, upekuzi wa mali chafu unaanzia kwa kutolewa Hati ya Upekuzi na Hakimu na hapo ndipo unapoanzia na wala mtu haendi tu kibabe, na kusema anataka kumsachi mtu.

Kwa sababu Hati hiyo ya Upekuzi inatolewa na Hakimu baada ya kupelekwa maombi ya kiapo na askari polisi yanayoelezea sababu za kuomba kutolewa kwa Hati hiyo ya Upekuzi. Hata hivyo, Hati hiyo ya Upekuzi haitolewi na Hakimu mpaka ajiridhishe kwamba kuna sababu za msingi zilizoorodheshwa kwenye Hati ya Kiapo na kutoa Hati hiyo ya Upekuzi.

Mhe. Mwenyekiti, haitowezekana kumpekuwa mtu kwa kumvua nguo bila ya kuwepo kwa Hati za Upekuzi inayotolewa na Hakimu. Suala hili naomba kulisisitiza sana. Lakini tukiangalia ile sheria yenyewe Mhe. Mwenyekiti, iimezungumzwa kwamba anaweza, yaani *may* na ikiwa, ama *if*.

Kwa hivyo, sio lazima na wala si kila kesi atavuliwa nguo, pamoja na mambo mengine, yaani *may* anaweza na *if* ikiwa. Mhe. Mwenyekiti, haya maneno ni *strong words* hapa na ninaomba tuyazingatie sana. Kwa kweli hii haimaanishi hapa, lakini wenyewe wataalamu wa wanasheria wanasema kwa taratibu lazima yawekwe, yaani kipengele hiki lazima kiwekwe na tukikiondoa kabisa si utaratibu.

Nafikiri Mhe. Abdalla Juma Abdalla alieleza jana kwamba kuna watu madawa ya kulevya wanaficha, wengine wanapasuliwa wanawekwa ndani. Sasa haidhuru kweli kuna vyombo vya kisasa vya *X-ray* pamoja vyengine. Lakini mtu amekamatwa huko mpaka unapojaribu kufungua kesi na kumpeleka na kutafuta *X-ray* na *CT Scan*.

Kwa hivyo, kwanza tuanzie na *physical inspection*, ambayo kama nilivyosema haitokuwa mtu yeyote lazima, lakini tumesema *may and if* na haya ni maneno mazito kidogo ambayo inafaa tuyazingatie kwenye sheria yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo lilijitokeza ni kuhusu kunyang'anywa mali, na Waheshimiwa Wajumbe wengi walilizungumzia hili. Kwa kweli kama nilivyosema wakati tunarekebisha labda kwenye marekebisho hayo mapya kama limetokezea suala hili basi ni kwa bahati mbaya tu, lakini naomba kusema kwamba kila kwenye kunyang'anywa mali isomeke kutaifishwa, hiyo hasa ndio madhumuni yetu. Kwa hivyo, kama limejitokeza tena kwenye mswada huu baada ya marekebisho iwe ni bahati mbaya, lakini hasa ndivyo tulivyokusudia.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la *Search Warrant* kwa kuzingatia maumbile ya makosa ya sheria hii, ili kuzuia kosa lisitendeke kwa kukosa *Search Warrant*. Hata hivyo, serikali imezingatia maelekezo ya Waheshimiwa Wajumbe na Jeshi la Polisi litaelimishwa ipasavyo juu ya suala zima la utekelezaji wa majukumu yao ya ndani ya sheria hii.

Kwa kweli kama nilivyosema Waheshimiwa Wajumbe wengi sana takriban wote walizungumzia suala la wasi wasi wa kutotekelezwa kwa sheria na kutokuwa na usimamizi wa kutosha. Mhe. Mwenyekiti, nathubutu kusema kwamba naomba niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe juu ya utekelezaji wa sheria hii.

Kwa hivyo, kama nilivyosema kwamba serikali imejidhatiti katika kusimamia kwa nguvu zote sheria hii, tukitilia maanani makosa mengi ya usafishaji wa fedha haramu na mapato yatokanayo na hayo. Adhabu zitatolewa kwa wale tu watakaopatikana na hatia, sheria hii haikutungwa kutokana na nguvu za nje, isipokuwa mazingira ya sasa ndiyo yanayotufanya na sisi Zanzibar tuwe na sheria hii.

Aidha sheria hii ni imani yetu kwamba itasaidia katika kudhibiti madawa ya kulevya hapa nchini. Mhe. Mwenyekiti, sheria hii kabisa haitotumika vibaya kwa ajili ya watu fulani na wala hatuna mtazamo huo hasa kwenye masuala kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Amri ya Kutaifisha na suala hili nakumbuka Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja alilizungumzia. Kwa kweli naomba nimshukuru Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kututanabahisha juu ya tafsiri hiyo.

Kutokana na hali hiyo mswada utafanyiwa marekebisho juu ya tafsiri hiyo na utasomeka amri ya kutaifisha, maana yake ni amri ya kutaifisha mali iwe ya kuhamishika au isiyohamishika. Kwa hivyo, tunakubali ushauri wake na ile tafsiri ya mwanzo kidogo ilikuwa haitoi tafsiri nzuri na wala haina mantiki inayofaa *(Makofi)*.

Vile vile Mhe. Ali Suleiman Ali alizungumzia juu ya suala la Wizara ya Fedha na Uchumi kushirikiana na wizara au taasisi nyengine zikiwemo Wizara ya Utalii, Biashara, na Uwekezaji. Ushauri huo tunaukubali tena ni mzuri.

Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema suala hili mkituachia peke yetu labda Wizara ya Fedha na Uchumi au Idara ya Mkurugenzi wa Mashataka ama *AG Chembers* au Jeshi la Polisi hatutoliweza. Hivyo ni vyema taasisi zote tunapaswa kushirikiana katika utekelezaji wa sheria hii japo kwa kutoa habari tu, basi itatusaidia sana.

Nikiendelea na majumuisho Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la kamari na bahati nasibu na hili nakumbuka Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi alilizungumzia kidogo. Kwa mujibu wa sheria hii nathubutu kusema kwamba kamari na bahari nasibu si miongoni mwa makosa yaliyoorodheshwa, ambayo

yanapelekea usafishaji wa fedha haramu yaani *predicate offence*, kwa hiyo hayana nafasi katika sheria hii.

Hata hivyo, tukiangalia kwenye ukurasa wa 63 kosa lililoorodheshwa maana yake kuanzia A mpaka Z na haya mawili hayamo. Kwa kweli namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum jana aliyasoma na kuyakariri vizuri tu makosa haya, yaani *predicate offence (Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la sifa za watendaji wa *FIU* na hili Waheshimiwa Wajumbe wengi walilizungumzia wakiwemo Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Ali Denge Makame, Mhe. Ame Mati Wadi, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na wengine wengi walizungumzia juu ya suala hili la sifa.

Kwa kweli sifa za watendaji zimeelezwa katika kifungu cha saba cha sheria hii ya Tanzania Bara, ambapo kifungu hiki kimependekezwa kiridhiwe na Baraza hili. Miongoni mwa sifa hizo ni pamoja na uzoefu katika masuala ya sheria, fedha, Forodha na Usimamizi wa Sheria na hizi ndizo sifa zenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na ushauri alioutoa Mhe. Rashid Seif Suleiman, kwamba katika utekelezaji serikali itoe taaluma kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu, kuwe na uadilifu na utekelezaji wa viwango vya kimataifa na kutolewa kwa mafunzo maalum kwa watendaji. Kwa kweli ushauri ni mzuri kama nilivyosema kwamba tumekubaliana na ushauri huo na tutajitahidi kujipanga vizuri, ili tuone utekelezaji wake unafanywa ipasavyo *(Makofi)*.

Vile vile kama nilivyosema suala jengine ambalo limejitokeza sana ni kuhusu adhabu, kama vile Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Ali Denge Makame, Mhe. Ame Mati Wadi, Mhe. Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba pamoja na wengine wengi walilizungumzia suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba adhabu katika sheria hii imezingatia ukubwa na athari za makosa husika. Kwa sababu kama nilivyoeleza hapo awali usafishaji wa fedha haramu unaathiri kwa kiasi kikubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hivyo, naomba ifahamike kwamba kusafisha fedha haramu hujipatia fedha nyingi kutokana na vitendo vya kihalifu.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana sheria hii ikatumia maneno isiyopungua adhabu husika, yaani mara nyingi huwa tunasema isiyopungua ile adhabu yenyewe iliyotajwa pale, ikimaanisha kwamba adhabu inaweza kutolewa zaidi ya kiwango hicho na wala si chini yake.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na suala zima la ufafanuzi wa mtu anayefariki takriban waheshimiwa wengi walizungumzia suala hili. Nafikiri ipo haya ya kulitolea ufafanuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, tafsiri iliyopo ni kwamba yule aliyefariki kabla ya amri ya kukamatwa haijatekelezwa uchunguzi utafanywa kama ilivyo kwa mtu aliyehai na endapo itathibitika kuwa na hatia hukumu dhidi ya mali yake kwa pale anapostahiki kutaifishwa au vyenginevyo itabaki kama vile mtu aliyehai anapohukumiwa. Naomba tuifahamu kwa mantiki hiyo na naomba tukisome kifungu kile cha 4(1c) mpaka 5 nafikiri itatoa ule mtiririko mzuri wa lile suala lenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 41 mtu mwenye hisa kununua tena mali iliyotaifishwa. Suala hili aliuliza Mhe. Ame Mati Wadi, Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niseme kwamba kufanywa kwa marekebisho badala ya mtu mwenye hisa isomeke mwenye maslahi. Hapo kidogo tumekubali *observation* zao na tunaomba kufanya marekebisho kwamba badala ya mtu mwenye hisa basi isomeke mwenye maslahi.

Mhe. Mwenyekiti, mfilisiwa anaweza kununua kwa vile ni haki ya kila mtu kununua mali iliyotangazwa kuuzwa ikiwa ni pamoja na huyo aliyefilisiwa. Kuhusu maana ya fedha haramu suala hili nakumbuka aliuliza Mhe. Haji Mkema Haji, Mhe. Ame Mati Wadi na waheshimiwa wengine wengi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hili tunakiri tumeona umuhimu wa kutoa siri ya fedha haramu haidhuru yale makosa yanayoletea kupata hizo fedha haramu tumeyataja lakini kweli maana yake fedha haramu tumehisi kweli inafaa katika maelezo hayo tuiweke. Kwa mtizamo wetu na kwa mtizamo wa sheria hii ni kwamba fedha haramu maana yake ni fedha au mali zinazopatikana kwa kujihusisha kwa mtu au watu moja kwa moja au vyenginevyo katika kubadili, kuhaulisha, kuficha, kuangamiza, kutumia, kuhodhi, kumiliki fedha au mali inayojuulikana kama sio halali na matumizi yake yanadhamiria kukwepa kutiwa hatiani kwa vitendo hivyo. Inajumuisha makosa iliyotaja katika kifungu cha 7 tumeyataja yale makosa na kama nilivyosema namshukuru Mhe. Zainab Omar Moh'd jana aliyasoma vizuri tu sitaki kuyarejea tena.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mkema tokea jana hata hii leo tunamshukuru kwa michango yake mingi ya ushauri, na kama alivyosema alikuwa na wasi wasi wa baadhi ya vifungu lakini namuhakikishia kwamba asiwe na wasi wasi na haya maelezo yake sisi tumeyasikia na tutayafanyia kazi. Mhe. Mwenyekiti, yeye alizungumzia zaidi suala la kulipa faini kwamba kifungu ni kizito. Hayo yote ukisoma kwenye marekebisho mapya ya sheria hii hayo yote yamewekwa kwa

uwazi kabisa na Mhe. Mkema bahati mbaya nafikiri alikuwa akisoma yale marekebisho makongwe. Hata hivyo katika matumizi ya sheria ya udhibiti ya matumizi ya fedha haramu kwa Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika udhibiti wa matumizi ya fedha haramu ni suala la kikanda ambalo linasimamiwa na jumuiya inayojulikana kama *Eastern and Southern Africa anti Money Laundering Group* yenye nchi wanachama 14 Tanzania ikiwemo.

Mhe. Mwenyekiti, karibu nchi nyingi za jumuiya hiyo tayari zimeshapitisha sheria kama hii, sasa tufikirie ikiwa Zanzibar bado hatujaipitisha tutakuwa wapi na athari zake ni zipi. Kwa hivyo, hili suala ni muhimu sana kwamba na sasa hivi hatuna budi sio kama kuna kishindo pia tuone kwa masuala haya ya uhalifu madhali wenzetu wameshapitisha basi inafaa na sisi tupitishe. Pia kwa kusisitiza ni kama alivyosema Mhe. Zainab jana aliyasoma yale masuala ambayo yanapelekea kupata fedha haramu na utaona yale makosa mengi takriban tunayo na yale yaliyokuwa hayapo basi yanakuja au wakati wowote tuyatarajie. Kwa hivyo, ni vyema tukachukua hadhari na mapema.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema tumejitahidi sana kuziweka pamoja hizi hoja za Waheshimiwa Wajumbe ili tuepukane na kumchambua mmoja mmoja. Lakini kwa ujumla tumejaribu sana kuchukua yale mambo makuu na makubwa naamini yatakidhi haja kama tumemsahau mtu mmoja basi sio dhamira yetu. Kwa mfano, watu wengi walichangia suala la ugaidi lakini suala la ugaidi hapa sio pahali pake hayo yametajwa kwenye sheria nyengine, lakini kama nilivyosema ushauri wao sisi tumeuchukua na tutayafanyia kazi kama ilivyofanyiwa kazi ile sheria ya mwanzo tukapata hii sheria mpya kabla ya kuanza kutumika kwake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nimalizie kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Uchumi kutoa shukurani za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao mizuri na naomba kwa nia moja tuipitishe sheria hii ili ianze kutumika nchini mwetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji wale ambao wanakubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili iweze kuupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu ya 2009

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Ufafanuzi
Kifungu 3 Taarifa ya kutiwa hatiani kwa kosa
Kifungu 4 Tafsiri ya kutoroka
Kifungu 5 Tafsiri ya kujishughulisha na mali
Kifungu 6 Mahakama kuhusika

Sehemu ya Pili

Katazo la Usafishaji wa Fedha Haramu

Kifungu 7 Tafsiri ya kuzuia usafishaji wa fedha haramu
Kifungu 8 Adhabu kwa kosa la usafishaji fedha haramu
Kifungu 9 Kosa lililofanywa na mashirika

Sehemu ya Tatu

Kitengo cha Upelelezi wa Taarifa za Fedha na Kamati ya Kitaifa

Kifungu 10 *FIU*

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake ila katika suala hili masuala ya *FIU* na ile kamati kwa kweli nahisi Zanzibar haikufanyiwa haki. Kwa sababu wajumbe ni 11 lakini Wazanzibari kuwa 3 hili ni tatizo wenzetu wakawa wako 8. Halafu katika kifungu hiki ambacho Mhe. Waziri jana alivigawa ghafla ghafla kama ni viambatanisho imesemwa kwamba *quorum* ni nusu, maana yake ni kuwa wenzetu wanaweza kufanya kikao na wakafanya maamuzi kwa sababu wao

wako 8 hata ikiwa sisi hatukwenda hata mmoja. Kwa hivyo, hatuoni kwamba kupitisha sheria ya aina hii ambayo maslahi ya Zanzibar hatukuyaona hivi Baraza nahisi haliwezi kuwafanyia haki Wazanzibari lakini naomba ufafanuzi zaidi kuhusu suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, *observation* za Mhe. Said Ali Mbarouk kwa kiwango fulani ni kweli kwamba *representation* yetu katika kamati hii ni ndogo na ndio maana hata kwenye kamati tukakubaliana na maelekezo ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba wizara ilifuatilia hili ili tuone *representation* yetu inaongezeka. Pia hata kwenye utendaji ile *FIU* ndio muhimu zaidi kwamba baada ya Kamishna wa *FIU* kama atatoka Tanzania Bara basi msaidizi atoke Zanzibar au vyenginevyo, hayo tumeyaona.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Saidi aangalie kwamba humu mna vyombo vya muungano kama Jeshi la Polisi ambacho ni chombo kikubwa cha nchi yetu. Lakini nataka nielezee kwamba watatu ni Taasisi za Muungano, Benki Kuu, Mambo ya Nje na Idara ya Usalama hizi ni taasisi za muungano ambazo zinatugusa mpaka sisi Zanzibar. Kwa hivyo, nakubali kwamba wakati mwengine tunatengwa lakini kwa kutarajia kwamba kuna moja kwa moja wanaotoka Zanzibar na kuna wale wa taasisi za muungano ambapo na sisi Zanzibar tumo humo. Mhe. Mwenyekiti, hayo tumeyaona tutazidi kuyapigania kwa nguvu.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Waziri nimeyasikia lakini uzoefu haoneshi hivyo, kwa kweli ingelikuwa uzoefu unaonesha hivyo tusingefika hapa kama tuna migogoro mingi ya muungano. Nina hakika Mhe. Waziri kwa imani ya moyo wangu kwamba tunapitisha kama Baraza hili mimi ningelisema kwamba kifungu hiki tusikipitishe mpaka pale ambapo kitafanyiwa marekebisho kuona maslahi ya nchi yetu yamekuwa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, vyenginevyo nina hakika hili litaingia katika kero za muungano na kuna siku tutaendelea kupiga kelele kwa mambo haya. Wenzetu katika mambo haya hawana ujomba wala hisani hawafikirii hata siku moja *interest* zetu wakaziangalia. Kwa hivyo, bado Mhe. Mwenyekiti namuomba sana Mhe. Waziri kwa maslahi ya nchi yetu hiki kifungu kweli kinaweza kikatuletea matatizo. Hata ukiangalia *FIU* wenyewe kuna suala la *appointing authority* hii pia ni wao ambayo imesema kwamba ime-*point such employees the appointing authority shall in particular every guard to person the experience in law finance custom and law enforcement.*

Mhe. Mwenyekiti, bado mimi kwa maslahi ya nchi yetu nahisi kwamba vifungu hivi vilivyo na ambavyo vimepitishwa na Bunge sisi tumeviambatanisha katika sheria yetu namuomba sana Mhe. Waziri aangalie kwamba hayatakuwa na mustakabal mzuri.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba mimi nimekubaliana na Mhe. Said kwamba *representation* yetu ni ndogo lakini nikiri kuwa suala lake tutalichukua na hili zaidi ni suala la kitendaji na sasa hivi tunashirikiana kwa pamoja. Kwa sababu hivi ninavyosema wao walitaka ile sheria tuliyoipitisha kule ifanye kazi kwetu, watendaji wakasema haiwezekani kwani hii tumepanga na tumekubaliana kwamba hilo haliwezekani.

Kwa hivyo, mheshimiwa mimi nathubutu kusema kwamba watu wetu walioko kule wameona wale wana sheria waliotoa masuala haya ni wanasheria waliobobea wanajua jinsi ya kulinda maslahi ya Zanzibar. Namuomba Mhe. Saidi atuamini kama anavyoendelea kutuamini siku zote na hili kama watendaji tutalifanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi ni swahibu wangu sana na anaelewa hivyo, kuna mambo huwa sina matatizo naye. Lakini matatizo yanayohusu *interest* ya nchi yetu kwa kweli mimi huwa mgumu sana kwa sababu tumeshatafunwa na nyoka mara nyingi kwa hivyo huu ni ukuti lazima utushitue. Kwa hivyo, ni ngumu sana kukubaliana na kipengele hiki na *hansard* bora inirikodi kwamba kuna siku tutakuja litia suala hili.

Kwa hivyo, bado mimi ni mgumu kukubali hili, ingelikuwa rahisi sana mimi kuruhusu tulipitishe lakini nashauri kwamba suala hili liende katika *the same charnel* tusiruhusu tu mambo ambayo nchi yetu itakuja kufika pahali ambapo tutajuta. Kama suala la haki za binadamu kulirudisha Bungeni likenda kufanyiwa *amendment* ambayo *interest* za Zanzibar zilikuwa *conceded* nadhani suala la fedha ni jambo muhimu sana. Kwa hivyo, hili ni suala ambalo muhimu wanaweza wakafanya maamuzi ambayo wasi-*regard* hali halisi wenzangu jana walisema masuala ya fedha zinazokuja kutoka nje wao hawapati.

Mhe. Mwenyekiti, nahisi ningeliishauri Kamati hii ya Baraza tukufu ikubaliane na mtazamo wangu kwamba suala hili tulirudishe ama mambo mawili. Tuunde FIU yetu na kamati yetu wenyewe au kama tunakubaliana na muungano basi iwekwe katika nafasi sawa kama watu 11 basi angalau tuwe watu 5 ili tuwanyime ile nafasi ya kusema wana *quorum.* Mhe. Mwenyekiti, tukiwapa *quorum* itakuwa tunajitia kitanzi ambacho nahisi watoto na wajukuu zetu watakuja kutulaumu kwa kutunga miswada ambayo tunawapa wenzetu nguvu

sisi tunajidunisha. Nakuomba sana Mhe. Mwenyekiti, kamati yako ikubaliane na hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hebu tuambie kitu gani ulisema unakubaliana na Mhe. Said Ali Mbarouk kwenye *point* gani unakubaliana nae.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saidi nakubaliana nae kwamba ukitizama kweli kwenye orodha hii (a-j) sisi hapa Zanzibar watatu ndio uhakika watu wetu. Hilo nakubaliana nalo kwamba kwa Zanzibar moja kwa moja wanaosema hawa wa Zanzibar mfano:

© *One representative of the Ministry of Finance of the Revolutionary Government of Zanzibar;*

(e) One representative of the Attorney-General's Chambers of the Revolutionary Government of Zanzibar

(f) Two representative of the Directorate of Criminal Investigation, one of whom shall come from its office in Tanzania Zanzibar;

Hao watatu moja hawa ndio wa Zanzibar. Lakini sasa ukitizama huku kuna mwakilishi Benki Kuu, kuna mambo ya nje hizi zote ni idara za muungano. Sasa kama Idara za Muungano basi Zanzibar hututoi, vile vile kuna Idara ya Usalama wa Taifa. Alichosisitiza kwamba hizi za Zanzibar tutazitetea pale kwa sababu hizi za muungano tayari sisi tumo, lakini kwamba tutunge yetu Zanzibar iwe ya kitaifa haitowezekana haya ni masuala ya kitaifa ni mazito.

Mhe. Mwenyekiti: Nafiikiri Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri anakubaliana na hii *composition* kama tunaupungufu, kwa hivyo kuna njia mbili. Kwanza kuunda yetu peke yetu haiwi lakini hii hii Mhe. Waziri anasema wao watajitahidi kupigania mpaka Zanzibar ionekane. Kwa hivyo, njia iliyokuwa bora kwanza ni kukitoa kifungu hiki na mkapiganie huko, mtafuzu mlete hiyo sheria. Kwa sababu kuunda sheria yetu wenyewe hiyo itakuwa tabu lakini ikiwa serikali inaona ni kweli tumepunjika basi watafanya hivyo. Sijui Mhe. Waziri unaonaje maana yake Mwanasheria Mkuu hayupo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, naomba tufungue ukurasa wa 70 kwenye sheria yetu kifungu cha 12(2) naomba kukinukuu.

> "Masharti ya sheria yaliyoelezwa chini ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki ambacho ni jadweli ya sheria hii yatalazimika kwa

matumizi yake hapa Zanzibar, kutokuwa yamerekebishwa moja kwa moja endapo yatafanywa marekebisho na Bunge".

Ni kwamba wao wakifanya marekebisho sio kama na sisi huku tufanye kwa hivyo usiwe na wasi wasi wowote hii sheria iko wazi kabisa kwamba *interest* zetu na uhalali wetu tunaulinda kwa sheria hii.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuisikia sana hoja ya Mhe. Said inamantiki kubwa sana na sisi kama Wajumbe wa Baraza ndio wenye mamlaka ya kukubali au kukataa kifungu. Kwa hivyo, kwa hoja hii hata mimi nimeshawishika, lakini kwa nini Mhe. Waziri huangalii ukurasa wa 56 wa kanuni naomba kunukuu.

Kifungu cha 84 (b):

> "Endapo waziri ataona kwamba anahitaji mapendekezo yoyote ya mabadiliko yafikishwe kwenye kamati anaweza kuomba mswada huu upelekwe kwenye kamati iliyopitia mswada huu au kamati nyengine yoyote itakayoamuliwa na Spika".

Hapa Mhe. Mwenyekiti, wewe ndio mwenye mamlaka na inavyoonekana Mhe. Waziri hajaona kwamba ayapate hayo mapendekezo, lakini sisi kama Wajumbe wa Baraza na tunajua uzito wake tunaelewa kero za muungano. Ningemuomba Mhe. Waziri akakikubali kifungu hiki kurejesha mswada kwenye kamati ili ufanyiwe mabadiliko ambayo sisi wajumbe tungeona yanafaa. Nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ame Mati Wadi kurejesha kwenye kamati kifungu hiki au kurejesha mswada?

Mhe. Ame Mati Wadi: Kurejesha kifungu sio mswada.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ushauri uliotolewa kwamba kifungu kurudi kwenye kamati kijadiliwe tena tunakubali kwa kifungu hicho.

Kifungu 11 Kamati ya Kitaifa
Kifungu 12 Kuridhiwa kwa vifungu

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, tukiridhia vifungu hivi maana yake ndio yale ambayo tumeyazungumza hayana tena nafasi. Kwa hivyo, hapo

ndio penye msingi wa suala hili, tukiridhia tukasema ndio maana yake yote tuliyozungumza hapa kwamba kamati inarudi itakuwa …

Mhe. Mwenyekiti: kifungu cha 11 na 12 vinakwenda pamoja na kile. Kwa hivyo, ni kitu kimoja. Tumeelewana?

Sehemu ya Nne

Usimamizi na Udhibiti wa Usafishaji wa Fedha Haramu

Kifungu 13	Mtoa taarifa kumtambua mteja
Kifungu 14	Mtoa taarifa kuanzisha na kutunza kumbukumbu za wateja
Kifungu 15	Mtoa taarifa kutoa taarifa ya uwekaji wa fedha wenye mashaka
Kifungu 16	Mtoa taarifa kuanzisha na kuendeleza utaratibu wa ndani wa kutoa taarifa
Kifungu 17	Kinga za ziada zinazohitajika kuchukuliwa na mtoa taarifa
Kifungu 18	Kumtahadharisha mtu
Kifungu 19	Kuondoa wajibu wa kutunza siri
Kifungu 20	Kinga kwa mtoa taarifa
Kifungu 21	Kusafisha fedha mipakani

Sehemu ya Tano

Kutaifisha

Kifungu 22	Maombi ya amri ya kutaifisha
Kifungu 23	Taarifa ya ombi
Kifungu 24	Marekebisho ya ombi
Kifungu 25	Kutolewa kwa amri ya kutaifisha endapo mtu atakuwa ametoroka
Kifungu 26	Utaratibu wa maombi
Kifungu 27	Amri ya kutaifisha
Kifungu 28	Amri ya kutaifisha mali
Kifungu 29	Athari za amri ya kutaifisha mali kwa mtu wa tatu
Kifungu 30	Kuondolewa kwa amri ya kutaifisha
Kifungu 31	Usajili wa amri za kigeni za kutaifisha

Sehemu ya Sita

Amri za Kulipa Faini ya Fedha

Kifungu 32	Kutumika kwa sehemu ya sita
Kifungu 33	Masharti maalum kuhusiana na makosa yaliyoorodheshwa
Kifungu 34	Amri ya kulipa faini
Kifungu 35	Makadirio ya faini
Kifungu 36	Mahkama kuondoa kinga kwa mashirika
Kifungu 37	Thamani iliyolipwa kutokana na amri ya kigeni ya mali iliyosajiliwa

Sehemu ya Saba

Kutaifisha kwa Mujibu wa Makosa Yaliyotajwa

Kifungu 38	Kutaifishwa kwa mali iliyozuiliwa
Kifungu 39	Kugomboa mali
Kifungu 40	Athari za kutengua kupatikana na hatia
Kifungu 41	Mtu mwenye maslahi kwenye mali iliyotaifishwa anaweza kuinunua tena
Kifungu 42	Uwezo wa kununua hisa nyenginezo kwenye mali zilizotaifishwa
Kifungu 43	Kutaifishwa endapo muhusika atashindwa kufikishwa mahkamani

Sehemu ya Nane

Usimamizi wa Mali Inayotakiwa Kutaifishwa

Kifungu 44	Uwezo wa kuepuka na kukamata mali haramu
Kifungu 45	Hati ya upekuzi wa mali haramu
Kifungu 46	Hati ya upekuzi inaweza kutolewa kwa njia ya simu
Kifungu 47	Upekuzi wa dharura
Kifungu 48	Majukumu kwenye mali iliyokamatwa
Kifungu 49	Kurudishwa kwa mali iliyokamatwa
Kifungu 50	Kupekua na kukamata mali haramu iliyotokana na makosa ya kigeni
Kifungu 51	Amri za kuzuia
Kifungu 52	Sababu za kutoa amri za kuzuia
Kifungu 53	Taarifa ya maombi ya amri ya kuzuia
Kifungu 54	Mtu anaweza kuhudhuria na kutoa ushahidi
Kifungu 55	Taarifa ya amri ya kuzuia

Kifungu 56 Mahkama kutoa amri nyengine
Kifungu 57 Mdhamini kulipa faini
Kifungu 58 Malipo kwa mali iliyozuiliwa
Kifungu 59 Usajili wa amri ya kuzuiliwa
Kifungu 60 Kwenda kinyume na amri yakuzuia
Kifungu 61 Majukumu ya mdhamini
Kifungu 62 Kinga kwa mdhamini kubebeshwa jukumu
Kifungu 63 Malipo na gharama za mdhamini
Kifungu 64 Mahkama kuondoa amri ya kuzuia
Kifungu 65 Kusita kutumika kwa amri ya kuzuia
Kifungu 66 Amri ya kuzuia muda kwa kosa la kigeni
Kifungu 67 Kusajili amri za kigeni kuzuia
Kifungu 68 Mdhamini kushughulikia mali iliyosajiliwa inayotokana na amri ya kigeni kuzuia
Kifungu 69 Hatua zinazochukuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka
Kifungu 70 Kuondolewa kwa amri ya kigeni iliyosajiliwa

Sehemu ya Tisa

Uwezo wa Kukusanya Taarifa

Kifungu 71 Amri za kuwasilisha
Kifungu 72 Kubadilisha amri ya kuwasilisha
Kifungu 73 Kushindwa kutekeleza amri ya kuwasilisha
Kifungu 74 Amri ya kuwasilisha kuhusiana na makosa ya kigeni
Kifungu 75 Uwezo wa kufanya upekuzi wa waraka
Kifungu 76 Hati ya upekuzi wa nyaraka za mali
Kifungu 77 Hati ya upekuzi wa makosa ya kigeni
Kifungu 78 Amri ya ufuatiliaji
Kifungu 79 Kuwepo kwa utumiaji wa amri ya kufuatilia kuweka siri
Kifungu 80 Amri za ufuatiliaji zinazotokana na makosa ya kigeni

Sehemu ya Kumi

Masharti Mengineyo

Kifungu 81 Katazo la kujishughulisha na mali haramu
Kifungu 82 Matendo ya Wakurugenzi, Maafisa, Wafanyakazi auMawakala
Kifungu 83 Kushughulikia mali zilizotaifishwa
Kifungu 84 Kima cha kuthibitisha
Kifungu 85 Rufaa
Kifungu 86 Gharama

Kifungu 87	Kutoathiri utumikaji wa sheria nyengine
Kifungu 88	Kuweka chini ya ulinzi
Kifungu 89	Kinga kwa upelelezi
Kifungu 90	Kanuni

(Baraza lilirudia)

UTARATIBU

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu kifungu cha 85 na 86 cha Kanuni ya Baraza. Wakati Kamati ya Baraza Zima ilipokuwa inajadili mswada huu imekubaliana kwamba vifungu vya 10, 11 na 12 virudishwe katika kamati iliyojadili mswada vifanyiwe marekebisho au kadiri itakavyokuwa. Sasa wakati kamati hiyo iliyojadili mswada huo haijakaa sijui utaratibu wa kupitishwa mswada huu utakuwaje. Tunaomba muongozo wa kiti chako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kwanza kabla sijatoa maamuzi nataka niwashukuru wajumbe namna tulivyoendesha Baraza leo na namna tulivyofanya mambo haya. Sasa vifungu vile vya 10, 11na 12 tumekubaliana viende kwenye kamati, lakini sio mswada mzima.

Mhe. Said Ali Mbarouk sasa kuna njia moja tuulizane, wale ambao wanataka vifungu vile viende kwenye kamati au wale wanaotaka mswada mzima uende kwenye kamati. Tuulizane. Lakini wengi tulizungumza hapa vifungu vile tu ndivyo vyenye utata viende kwenye kamati na waziri amekubali. Tumeelewana Mhe. Said? Kwa hivyo, tunachokipeleka kwenye kamati ni vile vifungu vyenye utata kikatiba vitapomalizika hapo nafikiri ni sawa sawa. Mhe. Waziri na Waheshimiwa Wajumbe tumeliona hilo?

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, samahani, muongozo ninaotaka utoke kwenye kiti chako ni kwamba baada ya kamati husika kukaa na kufanya maamuzi hatma ya Kamati Zima ya Baraza itakuwaje, hatma ya Baraza hili kukubaliana au kukataa na maamuzi ya kamati itakuwaje na hivi sasa *process* inayoendelea ni ipi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa *process* inayoendelea sasa hivi tunapitisha mswada huu lakini vifungu hivi vya 10, 11 na 12 tunaviweka *pending*, vitafanyiwa marekebisho baadae.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri baada ya majadiliano busara inayofuata sasa hivi tuahirishe Baraza hili kamati ikapitia vifungu vile tunavipitisha kwa pamoja mswada uwe umeshapita.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe asilipotoshe Baraza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri sio analipotosha anatoa mawazo yake, usiseme analipotosha.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Sawa naomba radhi. Ki utaratibu Mhe. Mwenyekiti kama ulivyosema, vifungu vyote vya mswada tumevipitisha isipokuwa vitatu. Sasa haya serikali sisi tutarudi tukafanye marekebisho yake. Kwa hivyo, leo hapa tunapitisha vifungu na mimi nitasema pale pamoja na marekebisho yake. Lakini tupitishe vifungu tumalize kazi, mswada mzima umepita wote.

Mhe. Haji Faki shaali: Mimi Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nina rai moja tu, na hii itakuwa ni fundisho kwa serikali yetu. Sisi tumeshalisema sana suala la Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mimi nina imani wamo watu wanayo rai lakini kwa *authenticity* ya rai hiyo itakuwa ndogo sana. Sasa mimi ushauri wangu uahirishe Baraza kwa muda wa nusu saa ukae na Spika na Washauri wa Baraza baadae turudi ukija itakuwa wewe na waziri mtakuja na msimamo uliokamilika. Huo ndio ushauri wangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi sasa hivi hapa ndiye Spika, mimi hapa ndiye ninayeongoza kiti, hakuna kipengele kinachonambia nikakae na Spika na Waziri mimi ndiye ninayeongoza Baraza naheshimu sana. Tulichozungumza ni mambo mawili, itabidi nipige kura. Moja tulizungumza kwamba sote tumekubaliana na waziri amekubali kuondosha vipengele vile vya 10, 11 na 12, atakaa na kamati atapotoa *ultimate* zake akishamaliza na kamati, wakati wowote atafanya *amendment.* Tunafanya *amendment* hapa.

Kesho tuna Mswada wa *SUZA* tunafanya *amendment*, sasa tusipoteze muda tumekubaliana na hoja nzito, sote tumeiona na ina utata lakini sote tumekubaliana. Mhe. Said Ali Mbarouk umetoa hoja yako waziri amekubali, na mimi nimetoa maamuzi sote tumekubali na sote tumeiona uzito wake. Kwa hivyo, sasa nafikiri tujenge ule umoja tulioujenga kwenye suala hili. Tukubaliane kuondosha vifungu vile baadae vitakuja. Mhe. Said tukubaliane hivyo.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze sana kwa busara zako za dhati kabisa katika uendeshaji wa shughuli zetu. Nampongeza pia mtoa hoja Mhe. Said Ali Mbarouk

ametutanabahisha jambo la msingi sana juu ya mustakabali wa Wazanzibari sote. Bahati mbaya kuna baadhi ya wajumbe huwa wana mwelekeo wa kuharibu huo mustakabal tunaokwendanao.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inapoleta mswada hapa *inclusion* kwa maana ya kuongezeka kitu ndani ya mswada ule baada ya kupitia kwenye kamati au kwenye Kamati ya Baraza Zima. Pamoja na kutoa kwa maana ya *omission*, ni utaratibu ambao wa kawaida ndani ya Baraza hili. Kwa hivyo, madhali waziri amekubali vifungu vile vitatu vitoke sasa amekubaliana na rai ya Baraza hili, haimaanishi kwamba mswada wake ule sasa una kasoro, atapohitaji yeye vifungu vile kuvirejesha atapitia tena kwenye utaratibu wa Baraza, Baraza limeridhia tutafanya *amendment* halijaridhia waziri atarudi navyo. Sasa Mheshimiwa haya yanayokuja hapa sijui yanatokana na jambo gani.

Ninawaomba sana Wajumbe wenzangu hikma hii, mwenendo huu na muongozo mzuri tulioupata kwa Mhe. Said Ali Mbarouk kwa mustakabal wetu hebu jamani twende nao tumalize shughuli hii kwa sasa. Vifungu vile tumeshakubaliana tuviache ndivyo alivyokubali Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, tumeshakubali kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, vifungu hivi tunaviacha na tunakwenda kuvifanyia marekebisho hapa vitarudi tena kwa kupata *amendment* ya Baraza.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwa rai hiyo nzuri na mimi naunga mkono huo utaratibu.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kidogo kwamba vile vifungu 10, 11 na 12 tunakubaliana kwamba katika mswada huu vinatolewa na inayobakia viendelee. Hofu yangu ni kwamba huko mbele ya vifungu vyengine vifungu vile vimekuwa vimetajwa tajwa. Sasa unaondoa mguu lakini kidole kinabaki huko mbele, ndio hofu yangu tu hiyo. Sasa mswada huu ambao unapitishwa marekebisho ya vifungu vile vitatu yanakwenda kufanywa, lakini ukipitishwa hapa ikitajwa ni kwamba sasa anapelekewa rais ku-*assent*, ana-*assent* kitu ambacho ni *almost in complete* kwa sababu kuna sehemu nyengine vimenyofuliwa. Hiyo ndio hofu yangu na naomba nilitahadharishe Baraza.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa tumesikia. Mhe. Said Ali Mbarouk uliyetoa hoja tunakushukuru kwa kuwa umekubaliana na wenzako wote. Na yako wewe Mhe. Hamad Masoud tumesikia, lakini mgonjwa kukatwa kidole awe ana mguu wote na mguu unafanya kazi. Sasa kitu muhimu si suala la kuchomoa, suala tumeshakubaliana hivi vifungu vitatu vitakwenda muamini waziri na vitakuja

baadae katika *amendment*, tubakishe vyengine tuendelee. Kwa sababu hili suala ni nyeti sote tunajua.

Hata mimi waheshimiwa *Wallahi* siku za mbele hakuna kazi tabu kama ukiwa *back bencher* halafu kukaa hapa. Kwa sababu unataka kucheza, unataka kutia mguu inakuwa ni kazi kweli. Mimi kwa kweli siku ninayokaa hapa naona shida sana, kwa sababu unataka kuchangia na wewe unaona kitu hivi ni tabu sana. Kwa hivyo, mwenzenu nioneeni huruma mimi mwenyewe lakini nimo. Ni mwenzenu jamani. Haya sasa nafikiri tumemaliza hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa busara zako pamoja na Baraza zima kwa kutuweka katika mstari uliokuwa mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyanyue mikono juu. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Halisi ya mwaka 2009

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato halisi ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyanyue mikono juu. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ulisomwa mara ya pili na kupitishwa))

TAARIFA

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nina taarifa fupi tu muhimu ili nataka *hansard* ikae inihukumu. Wakati nilipotoa ushauri wa kuahirisha Baraza kuna watu waliguta sana, wakakejeli sana, lakini ilikuwa ni haki yangu chini ya kifungu cha 64 cha Kanuni zetu za Baraza ambacho kinasomeka hivi, "Mjumbe mwenye sababu ya kutaka kuahirisha mjadala wowote unaoendelea anaweza kutoa hoja kwamba mjadala uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe mpaka wakati gani". Sasa mimi nilifanya hivyo chini ya Kanuni ya 64(1) wala haikuwa kwa sababu nyengine yoyote.

Sasa kwa sababu ya kuweka *hansard* sawa napenda hili niliweke wazi kwamba ilikuwa ni haki yangu kwa mujibu wa kanuzi zetu za Baraza.

Mhe. Mwenyekiti: Kwanza nataka kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote ambao tangu jana jioni nimeingia mimi mpaka leo kuendesha Baraza hili. Mnajua kwa nini jana nikaingia? Jana nimeingia kwa sababu Mhe. Spika, alinambia jioni niingie kulikuwa na wachangiaji 8 tena wa kukamatia kamatia. Unajua kwa sisi watu wa mjini kukamatia lugha mbaya, mimi hakuna niliyemkamatia wote wamenijia wenyewe. Sasa nashukuru tumefika wajumbe 20 wamechangia.

Faida ya kuchangia wajumbe hao ni nini? Mswada wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji umechangiwa na watu wanane, lakini mswada uliofuatia hapo ambao ulikuwa na semina ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii watu 16, Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi watu 17 kwa sababu waliandaa na huu ulifanyiwa semina vile vile, watu 20 wamechangia.

Kwa hivyo, napenda kusema sana uzuri sana hii miswada inapokuja iwepo mipango ya semina watu waelimishwe, watu wafahamu, na mmeona leo namna gani watu walivyofanya.

Pili nakushukuruni kwa dhati kabisa kwakunipa leo shahada ya kuweza kuongoza mjadala huu, mimi leo ni furaha kubwa kwangu, nimeweza kuuongoza mjadala huu na tumepata muwafaka. Nafikiri ninaweza.

Vile vile nataka nitoe shukurani zangu kwa wajumbe, mimi kuanzia Januari, 2006, 2007, 2008, 2009 Baraza hili mpaka 2010 mimi namsaidia Mhe. Spika na nyinyi mnanisaidia mimi. Nakushukuruni sana kwa miaka minne niliyomsaidia Mhe. Spika kufikia sasa hivi. Nasema haya ndani ya moyo wangu sio kazi rahisi kukaa hapa. Mimi nafunga bila ya kupata thawabu, siku za Baraza mimi sili kabisa, kwa sababu sikujua saa ngapi, kwa sababu mimi naambiwa tu, njoo jioni, njoo asubuhi, njoo saa ngapi, lakini *Alhamdulillah* nashukuru. Namshukuru sana Mhe. Spika kwa mashirikiano aliyonipa na uzoefu na Mwenyezi Mungu ndiye ataemlipa heri hii. Na nyinyi ndugu zangu vile vile tuendelee kushirikiana.

Sasa nimeona niseme haya leo kwa sababu kesho ni binadamu naweza kuwa nisiwepo naweza kuumwa. Nakushukuruni sana sana na tuendelee kushirikiana na hili tulilolifanya sasa hivi huu ndio msimamo wetu katika mambo ya nchi yetu. Hiyo ni wazi natoa wazo kuwa ni msimamo wetu huu ndio uungwana. Kwa hivyo, nakupongezeni sana, sana, sana. Sasa kwa kazi nzuri sana iliyofanywa namuomba Mhe. Waziri aje aahirishe kwa sababu wakati bado haujafika.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Mwenyekiti, samahani sana sijakusudia kusema jengine lolote, isipokuwa nakusudia kwamba nimeleta taarifa yangu hapo nilikuwa naomba uwatangazie Wajumbe wangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwamba, kutakuwa na kikao cha kamati saa saba mchana katika ukumbi wa juu.

KUAkHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Baraza lako tukufu tumekamilisha shughuli zote zilizopangwa kwa leo na kuzifanikisha pamoja na kuzikamilisha kabla ya wakati wake, naomba uliahirishe Baraza lako tukufu mpaka kesho tarehe 28/10/2009 saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya kuwa Baraza hili liahirishwe mpaka kesho saa 3:00 asubuhi wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 5:33 asubuhi Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 28/10/2009 saa 3:00 asubuhi)